**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baiskeli Dar es Salaam**
**Tarehe 4 Augusti 2007**

**Waliohudhuria**
Abdallah Khatib
Ally Saidi Mohamedi
Ally Saidi Mwishekh
Ally Salum
Benison Ngiliule
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Juma Ali Salehe Jongo
Jumanne Idd Selemani
Kassim Bakari
Kibwana Mohammad Msiga
Lameck Charles
Mfinganga
Mohamed Salum Athman
Muniko Chacha
Mussa Omari
Patrick Masinga
Rahma Ali
Ramadhani Rajabu Nyengo
Rashidi Saidi Karanji
Sudi Saidi
William Samweli

**Msafara wa Baiskeli**
Bwana Mlamba wa AALOCOM alisema kuwa wawakilishi wa AALOCOM wa kamati ya msafara watakuwa Bwana Nyoni, Prosper nay eye mnwenyewe. Elaine aliwapigia simu lakini hakuna aliyekuwa tayari kuhudhuria kwenye mkutano siku hii saa tatu asubuhi hivyo aliahirisha kikao na wawakilishi wa CHABADA hadi wiki ijayo. Bwana Nyoni alisema atafuatilia kujua ni kiasi gani cha fedha kitatapatikana toka ITDP Elaine pia alituma barua pepe kwa Bradley wa ITDP kuthibitisha lakini hajapokea majibu.

Bwana Bkhresa na meneja wa Knight Support wako nje ya nchi kwa sasa. Elaine aliambiwa kwamba meneja wa Knight Support atarudi jumatatu na Bwana Bakhresa atarudi tarehe 16 Agusti. Juma alipeleka barua Celtel kuomba ufadhili.

Juma alipeleka barua kwa mbunge Azam Zungu kumwalika awe mgeni rasmi wa msafara. Aliambiwa apige simu tena ofisini baada ya wiki mbili ambapo mbunge atakuwa amerudi toka bungeni Dodoma.

Tazama chini michango ya guta kama zawadi ya bahati na sibu ya msafara wa baiskeli.

**Ofisi**
Mchango ulifanywa kwenye mkutano na Tsh 21,000 zilikusanywa ili kupaka rangi na kuweka samani ofisini. Ally saidi Mohamad alisema atachangia muda wake kupaka rangi pamoja na mwanachama mgeni Rahma Ali, pia atachangia brashi ya kupaka rangi. Alipewa Tsh 10,000 toka kwenye fedha zilizochangwa kwa ajili ya kununua rangi. Juma alihifadhi kiasi kingine cha fedha kilichosailia.

Elaine alipitisha picha toka internet ya kuwekea nyaraka / magazeti na Ally Saidi alisema atapeleleza in kiasi gani itagharimu kutengeneza.

Tazama chini kuhusu guta kukidhi mahitaji ya kodi ya ofisi.

**Kutembelea kampuni ya kutengeneza Guta**
Jumatatu sudi Saidi, Paulo Atibu, Elaine na Juma walitembelea meneja wa kampuni ya kutengeneza guta Mhe Ngaja alitufahamisha kuwa Guta inamaanisha “Gurudumu tatu”. Kampuni ilianza kutengeneza Guta mwaka 1970 kutokana na wito wa Mwalimu Nyerere kuhusu njia za usafirishaji mizigo rahisi kwa watu wa kawaida. Kampuni iliandaa guta, mwanzoni watu hawakuyazoea ila baada ya kuona linayotumika walizoea. Mhe Ngaja aliunga mkono shughuli za UWABA. Pia alitutambulisha kwa mwanae wa kiume.

Tulielezea pendekezo la UWABA kuwa na Guta kwa ajili ya kupata fedha za kodi ya ofisi alidsema atatuuzia Guta kwa bei nafuu Tsh 280,000.

**IBike**
Jumanne mchana kundi la wanachama wa UWABA walikutana na watalii wane wamarekani wa IBike waliotoka Zanzibar na kupand nao baiskeli hadi Mabibo, ambako tulibadilishana mawazo. Jambo hili lilikuwa la kufurahisha kwa watalii na kwa wanachama wa UWABA moja ya mambo yaliyozungumzwa ilikuwa kukosekana kwa wanawake katika UWABA – watalii wote wanne walikuwa  wanawake. Mambo mengine yalikuwa kuhusu upandaji baiskeli Tanzania na Marekani na tofauti ya matumizi ya baiskeli Tanzania, mazingira na mabadiliko ya hali ya hewa. Tulikutana pia na waongoza watalii yassin na said Idd Shandala. Yassini anaishi Tanga na aliongelea kazi yake ndani ya IBike, kupanda baiskeli Fanga na shirika jingine lisilo la kiserikali nani mwanachama. Saidi Idd anaishi Dar es Salaam kwa muda na alijiunga na UWABA.

IBike alipendekeza kupitia barua pepe kuwa UWABA ikutane na watalii wengine wa IBike wakati ujao.

Yassin ataweka Tsh 400,000 benki ambazo ni mchango wa IBike kwa UWABA watakaporudi toka safari yao.

**Barabara zilizo kwenye mpango wa ujenzi**
Elaine alipiga simu makao makuu ya TANROADS ili kupanga mkutano na Bwana Nitti lakini bado hakuwepo ataendelea kujaribu kumpigia.

**Sanduku la posta**
Juma alifuatilia posta akaambiwa kwamba kufungua sanduku la shirika litagharimu Tsh 37,000. hata hivyo kwa vile hakuwa na hakika ni kiasi gani hutolewa kwa mara moja na ni kiasi gani kwa mwaka na gharama za picha au nyaraka. n.k. atakwenda tena wiki ijayo na orodha ya maswali.

**Mpango wa Usafiri Dar es Salaam.**
Filbert alisema atafuatilia barua yetu kuhusu mada hii katika chuo cha usafirishaji Dar es Salaam.

**Mengineyo**
Wajumbe zaidi walichukua vimbulisho na kutoa mchango Tsh 500 kwa gharama za utengenezaji.

Elaine alisema ametuma barua pepe Africa ya kusini, shirika liitwalo Ben Bikes na kujadili jinsi tutakavyoshirikiana.